

JINYENYEKEZE



[Ndugu Neville anamjulisha Ndugu Branham—Mh.]

Sasa naamini ningeweza kufanya matangazo basi, “Kuna vipawa fulani: vya mimi kuwazia jambo kama hilo.” [Ndugu Branham na mkutano wanacheka.]

² Hakika mimi nafurahia kuwa hapa kila wakati. Safari yetu inakaribia mwisho sasa, wa sisi kukaa nanyi. Maana, tuna mkutano mwingine unaokuja sasa hivi huko Chicago, nami sina budi kuirudisha ja—jamaa yangu Arizona mara niwezapo. Nao hawajapata likizo yao ya msimu wa kiangazi bado, nami ninapaswa kuwapeleka mahali fulani kwa motokaa, mnamo siku chache. Halafu labda nitaondoka kwa siku moja, moja, moja ya Jumapili, kisha juma lifuatalo nitaanzia Chicago. Kisha itanilazimu kurudi moja kwa moja, Jumatatu, na kuwapeleka Arizona.

³ Na sasa nachukia kuja mnamo Jumapili asubuhi, kuchukua wakati huo ambapo kila mtu ameburudika. Jumapili usiku, daima umechoka na kudhoofika, Jumapili usiku; halafu nampa ibada ya Jumapili usiku mchungaji wetu, hivyo—hivyo kwa namna fulani ni vibaya. Bali nachukia kufanya hivyo, na hata hivyo Jumapili usiku ningeichukua, Jumapili usiku, kufanya ibada Jumapili usiku, halafu nawachelewesha watu sana. Wengi wao wanakuja humu kutoka mbali kusini na—na huko mbali kaskazini, nao wana, loo, wakati mwingine wanaendesha magari usiku na mchana, kusudi tu wapate kufika hapa kwa ajili ya ibada moja, kisha wanarudi. Na hiyo ndiyo sababu najaribu kuwahi Jumapili asubuhi, ninapokuja, kuwapa nafasi ya kurudi.

⁴ Wasafiri waaminifu na wanyofu, jinsi ninavyowathamini! Wanaendesha kwenye mvua ya theluji, mvua, na kila kitu, ili wafike hapa, kupitia nchini, mamia ya maili, kwa ibada moja dogo tu. Kwa hiyo inanifanya nijisikie kumshukuru Mungu, na kwa watu hawa, kwa ninino yao kuu—kwa usaidizi wao mkuu, na yale ninayotaribu kusema, kwa watu, kuwa ni Kweli.

⁵ Naam, naamini hii kuwa ni Kweli, mimi...kwa moyo wangu wote. Kama kungekuwa na lingine lo lote, ambalo nilidhania ni bora zaidi, bi—bila shaka ningenda kwanza... Nisingemwomba mtu ye yote aende mahali po pote ambapo nisingenda kwanza, kuona kama ni kweli au la. Nisingemwomba mtu ye yote ku—kupiga hatua, katika Mungu, ambayo sikuwa nimeshapiga na kujua kwamba ni Kweli. Kwanza, sharti iwe ni Neno la Bwana, kisha sharti nipige hatua na kuona kama ni sawa. Ndipo, kama ni sawa, basi naweza kusema, “Njoo huku.” Mnaona, ni kutayarisha njia.

6 Na, sasa, nafikiri mhudumu ye yote anapaswa kufanya hivyo, anapaswa kwenda kwanza, yeye mwenyewe. Anapaswa kuwa kiongozi, kiongozi wa watu, asizungumzie jambo ambalo hawezi kuligusa kwa mkono wake, yeye mwenyewe. Tunapaswa kutoka kwenda kule, viongozi wa watu.

7 Asubuhi ya leo, nilipata ujuzi wa kipekee na wa kigeni sana hapa mimbarani. Na hiyo ilikuwa, karibu sehemu ya mwisho ya Ujumbe, sikukusudia kuisema hivyo. Mnaona? Bali nakisia tayari imesemwa, na hakuna ninaloweza kusema juu yake sasa. Ila basi nilienda nyumbani, nikaanza kusoma habari zake.

8 Halafu tulikuwa na mkutano mdogo wa jamaa leo, wa ndugu yangu tu na hao wengine. Mama ameaga dunia. Nasi tulizoea kukutana kwake, na sasa tunaenda kwa Delores. Tulikuwa na wakati mzuri kule alasiri ya leo, tukizungumza, naye Teddy alikuweko na akaimba nyimbo, akacheza nyimbo kadha na kadhalika.

9 Sasa nafikiri, labda Jumapili ijayo asubuhi, kama Bwana akipenda, iwapo Ndugu Neville hajali, sasa ningetaka kufanya ibada ya kuponya, ibada maalum ya kuponya tu. Nami—nami nafikiri, juu ya Ujumbe asubuhi ya leo, jinsi ilivyoelekea Bwana alikuwa akiniongoza kuuleta, kueleza, inapaswa kututia moyo kidogo, mnaona, ku—ku—kuamini kweli. Tu—tunachezacheza, na tu—tunasema mambo mbalimbali na kuyazungumzia. Bali inapofikia uamuzi wa mwisho, hilo ni jambo tofauti. Kama vile. . .

10 Mtu fulani alikuwa akiniambia, naamini ilikuwa ni ndugu yangu kule nyuma, alikuwa akiniambia ha—hadithi ndogo leo, juu ya mtu, m—mhudumu na ninino yake. . .baadhi ya, mmoja katika kusanyiko lake. Naye akasema kwamba angeweza kutembea juu ya gogo.

Akasema, “Mchungaji, hakika, Mungu yuko pamoja nawe.”

Akasema, “Naweza kubeba gogo mgongoni mwangu, ninapovuka.”

“Hakika, Bwana yu pamoja nawe.” Kisha akaenda akafanya hivyo.

11 Akasema, “Naweza kubeba gogo, na kusukuma wilibaro nikaivusha, wakati uo huo.”

12 “Hakika, mchungaji, Bwana yu pamoja nawe. Imani yako inaweza kufanya lo lote.”

13 Akasema, “Naweza kukuweka kwenye hiyo wilibaro, na huku ninalibeba hilo gogo.”

Akasema, “Sasa, hebu ngoja kidogo!” Mnaona?

14 Ni tofauti unapohusika, wewe mwenyewe. Mnaona? Sasa, hilo, ni vizuri sana kwetu kusema hapa, “Amina.” Ni vizuri sana

kwetu kusema, “Naamini hilo ni kweli.” Bali hebu litekeleze. Inakubidi kulitekeleza.

¹⁵ Kama nilivyoleta tamshi hilo asubuhi ya leo, watu walikuwa wakilala kwenye kivuli cha Petro, hata hawakuomba waombewe.

¹⁶ Nimeingia katika nyumba nyingi, nikiangalia hili. Naomba kabla ya kuondoka, ndipo ninaingia mle nikiwa na upako, na hata siwaombe watu, kisha naenda zangu nao wanaponywa. Mnaona? Mnaona? Hiyo ni kweli. Nimeona likitendeka mara nyingi sana! Mnaona? Inakubidi kuwa na mahali fulani ambapo utaiweka imani yako. Unaona? Huna budi kuliamini. Nami naamini ya kwamba wakati huo unawadia, nao ndio huo.

¹⁷ Nami natambua kwamba hii siyo ibada ya kanda. Huenda wakajinasia moja ndogo, bali hii siyo kanda inayosambazwa nchini kote. Ile . . .

¹⁸ Hili ndilo nililokuwa ninazungumzia asubuhi ya leo limetuleta hata kwenye—kwenye kilele, na hiyo ndiyo sababu nitachukua Jumapili ijayo kwa ajili ya—ya—ya ibada ya kuponya. Kwa sababu, tangu nimekuwa nyumbani, nimewaambieni juu ya maono na yale yametukia, na kila kitu, na kulileta moja kwa moja, kwa nini mimi nimefanya mambo haya yote. Ndipo asubuhi hii, nalileta moja kwa moja hata kwenye Mvuto huo wa mwisho.

¹⁹ Sasa ni wakati wangu wa kujiweka wakfu kwa Mungu; wakati wa Mungu kunena nami. Mnaona, la—la—lazima nipate badiliko kidogo katika maisha yangu. Si kwamba ninafikiria ati mimi ni mwovu, bali na—nataka kujisikia niko karibu zaidi na watu. Mnaona?

²⁰ Watu ambao nimejaribu kuwaambia hii Kweli ya Injili, nao wanaipa kisogo, na kuondoka na kuidhihaki. Sasa, kwangu mimi, hiyo inaonekana kama ni tusi. Sijali, kwangu mimi; bali kwa mambo ambayo nimekuwa nikisema, ni Kweli nikijaribu kuwasaidia. Kama kuisukuma boti, na kusema, “Hii, hii hapa, vuka! Hii hapa, toka kwenye huo mto unaofurika, utakufa! Wewe, utaangamia pale!” Nao wanakucheka tu, na kuondoka. Vema, kwangu mimi, inaonekana kana kwamba, kama wakiondoka, hakuna la zaidi ninaloweza kufanya juu yake, mnaona, ninaloweza kufanya.

²¹ Bali nataka kukimbia ukingoni sasa na kuwashawishi, “Rudini!” Mnaona, sina budi kuwa na hisi ya namna hiyo, mnaona, kwa maana najua kuna mtu huko nje ambaye bado hajaingia. Nami ni—nitavua samaki hata . . . Yeye alisema, hata samaki wa mwisho atakaposhikwa. Nataka kufanya hivyo sasa.

²² Na sasa, ili kufanya jambo hili, ninatarajia jambo fulani kutukia katika mstari wa maombi. Jambo fulani . . . Na wengi wenu mnakumbuka lile ono la—la ule Mvuto wa mwisho, ule Mvuto wa Tatu, hasa. Mnakumbuka, kuna jambo lililotukia

kabla tu ya jambo hilo: niliona Nuru ile ikija na kuingia mahali pale, na kusema, “Nitakutana nawe mle.” Sasa natazamia jambo fulani kutukia.

²³ Hapa miaka mingi iliyopita, ilikuwa kwamba ibada na upambanuzi huo ungenifanya niwe mnyonge sana hata ningeyumbayumba. Wengi wenu mnakumbuka jambo hilo. Ingefikia mahali ambapo ningesimama huku Jack Moore yuko kwenye mkono mmoja, na Ndugu Brown kwenye mwingine, na kunitembeza huku na huko barabarani, kwa saa moja baada ya ibada. Basi nami, ikawa tu kwamba, nilikuwa nikijaribu kufikiria mahali ambapo—ambapo nilikuwa na yaliyokuwa yanatukia. Halafu, usiku mzima nalala pale na kuwazia habari zake, na kulia kwa kwikwi na kila kitu, na kushangaa kwa nini hawakumpokea Bwana wetu Yesu.

²⁴ Kisha akaniambia ono, “Wakati mmoja utakutana na bibi atakayekujia, amevalia suti ya hudhurungi, naye atakuwa amembeba mtoto mchanga kwenye blanketi, na tangu wakati huo na kuendelea, utapata nguvu ya kuvumilia zaidi.” Vema, niliwaambia yote hayo. Lilitukia huko Chicago, usiku huo wakati maskini bibi mdogo wa Kipresbiteri, wakati mchungaji wake mwenyewe alipomtuma kule na mtoto.

²⁵ Nami naamini ilikuwa ndugu yake, ama mmoja wao, a—alikuwa daktari. Akasema, “Hakuna matumaini kwa mtoto huyu mchanga isipokuwa Mwenyezi Mungu amguse.” Akaenda...

²⁶ Akaondoka akaenda akamwambia mchungaji wake. Mchungaji akasema, “Mi—mimi siwezi,” akasema, “ku—kutekeleza huku kuponya Kiungu, kwa sababu mimi si... haimo ndani yangu, imani inayohitajika kutekeleza.” Sasa, huko, huko ni kuwa mwaminifu kwa jambo hilo. Mnaona? Akasema, “Haimo ndani yangu kabisa.” Akasema, “Lakini nilikuwa katika mmoja wa mikutano ya Ndugu Branham, nami ningetaka kukushauri umpeleke mtoto huyo kwa Ndugu Branham.” Na daktari alikuwa amemkatia tamaa, naye alikuwa yuaenda kufa.

²⁷ Ndipo maskini bibi huyo akaingia mle ambamo nilikuwa nikifanya na—namna fulani ya ibada kwa ajili ya wale watoto wadogo Wakatoliki ambao walikuwa wameungua moto, kwenye ile shule kule, mwajua. Mnakumbuka ilikuwa wakati gani. Tulikuwa tukifanya ibada hiyo, ndipo maskini bibi huyu mwenye suti ya hudhurungi anashuka akija jukwaani. Mke wangu na hao wengine walikuwa wameketi pale, ndipo nikasema... nikageuka nikaangalia, na nikaangalia kila mahali, na kuona kana kwamba walikuwa wamesimama pale. Na ikatukia kuwa, kwamba kabla tu sijafika, naamini Billy Paul na hao wengine walikuwa wanamzungumzia, ama mke wangu ama hao wengine, na huyu bibi mwenye huyo mtoto mchanga.

Kisha huyo bibi akapanda akaja jukwaani, naye Roho Mtakatifu akafunua jambo lote, kisha akamponya mtoto huyo pale.

²⁸ Nikaondoka nikaenda zangu, na tangu wakati huo sichoki. Mnaona, hainisumbui, nami ni—ninaendelea moja kwa moja.

²⁹ Sasa ninatarajia jambo fulani kutukia, kuuelekeza huo Mvuto wa Tatu kwenye lengo, mnaona, na huenda ikawa ibada ya kuponya ya asubuhi ya Jumapili ijayo labda itasababisha jambo hilo. Sijui.

³⁰ Nafikiri, litupasalo kufanya, ni kuwaambia watu, kuwaleta wagonjwa. Naam, kwa ajili ya ibada ya kuponya, inatubidi kujiweka wakfu kwa ajili ya wagonjwa. Waleteni watu wenu walio wagonjwa, na muwalete hapa jumapili ijayo asubuhi na mapema, tuseme yapata kama saa mbili ama saa mbili na nusu, nasi tutawaacha wawape kadi za maombi wanapoingia mlangoni, namna yo yote ile watakayofanya. Ndipo tutakapopanga mstari wa maombi na kuwaombea wagonjwa, tuone tu atakayotenda Roho Mtakatifu.

³¹ Naamini Yeye atafanya maajabu kama tu tutamwamini, mnaona. Bali hatuna budi kumwamini kwa ajili ya jambo hilo sasa, kwa mioyo yetu yote. Nami nafikiri ya kwamba ile saa iliyo kuu imewadia ambapo Mungu, kama tulivyokuwa tukizungumza asubuhi ya leo, ametuonyesha mambo mengi sana, na kutuleta kwenye ninino fulani. . . kutufikisha tu mahali fulani. Kutupandisha tu kwenye kilima kile kidogo, na hilo tu ndilo tunalohitaji, halafu mambo yanaanza. Mnaona, i—inaendelea tu kama ilivyokuwa, jambo lile lile, na upambanuzi, jambo lile lile kwa kinabii, kuangalia.

³² Nilikuwa nimesimama kule Calgary. . . Samahani, ilikuwa queen city, kule chini Regina, Regina. Naye Ern Baxter alikuwa amesimama pale, na baadhi yetu. Na Bwana aliishaniambia, papa hapa jukwaani, “Itakuwa kwamba, utajua siri za mioyo yao.” Na hiyo ni kweli. Nami sikuwazia jambo hilo kwa njia hiyo. Nilipanda nikaenda jukwaani usiku huo, pamoja na Ern, na kuanza tu kuwaombea wagonjwa. Ndipo hapa yuaja mwanamume, maisha yake yote yakawekwa tu wazi; mara ya kwanza ilipotendeka jinsi hiyo, katika dakika moja, katika ibada ya kuponya. Kisha nikaangalia kwenye mkutano, na hapa ikaanza kuja kwenye mkutano na kadhalika. Loo, tutakapofika ng’ambo ya pili! Nusu bado haijasimuliwa, ya mambo hayo, kutoka kwenda na kuona mambo katika maisha ya watu. Sisemi neno juu ya jambo hilo. Naliacha tu peke yake, unaona, isipokuwa nimeshurutishwa kweli kusema neno.

³³ Na sasa natazamia jambo hili lingine kuanza namna hiyo. Mnaona, Mungu, katika njia Yake Mwenyewe, katika wakati wa mamlaka Yake Mwenyewe, kuanza jambo hilo. Na itakuwa—itakuwa jambo jingine ambalo litakuwa—litakuwa juu zaidi

ya watu hawa wengine. Mnaona? Nami natazamia jambo hilo kutukia.

³⁴ Na huenda ikawa, loo, niliwazia, kama ninge kuwa na ibada ndogo ya kuponya labda Jumapili ijayo. Halafu Jumapili ifuatayo labda nitakuwa nimeondoka pamoja na watoto na hao wengine, maana hawana budi kurudi kusudi waende shuleni. Halafu Jumapili ijayo, mimi, bila shaka, niko kule Chicago, kwenye mkutano kule. Kisha nitarudi Jumatatu ijayo, ndipo niondoke Jumanne niki—nikielekea Arizona, ambako watoto watarudi shuleni.”

³⁵ Vema, ulipata nini, mchungaji? [Ndugu Neville anasema, “Vema, nimevumbua kitu fulani cha ajabu sana.”—Mh.] Vema, hilo ni sawa kabisa, sasa tunataka kusikia habari zake.

³⁶ Kwa hiyo sasa Bwa—Bwana awabariki nyinyi nyote, sana. Na—nami nataka kuwaona Jumapili ijayo. Na Jumatano usiku. . .

³⁷ Pia sikizeni. Msiyasahau makanisa haya madogo, kama la Ndugu Ruddel, Ndugu Jackson, Ndugu Parnell, na hao maskini ndugu ambao wanajitahidi sana kule, mnaona. Nao wanajisikia kama kwamba sisi ni kanisa linaloshirikiana nao—nao—nao hapa, mnaona. Sisi ni kama kudi ndogo ambalo ni mama kwao. Hapo ndipo walipozaliwa, kutoka hapa, wachungaji na kadhalika.

³⁸ Na maskini jamaa huyu huku nyuma, ndugu, nilikutana naye juzijuzi usiku kule, Allen, maskini Ndugu Allen. Natumaini Ndugu Collins hapa atamwendea Ndugu Allen, iwapo hamjui. Wote wawili ni wahudumu wa Kimethodisti, nao—nao wameona Kweli ya Neno.

³⁹ Ambapo, ma—madhehebu ya kanisa la Kimethodisti, ambamo kuna kundi zuri la watu katika kanisa hilo la Kimethodisti. Usidhani kamwe kwamba si wazuri. Ni wazuri. Wao ni kundi la watu wazuri katika kanisa hilo la Katoliki. Wao ni kundi la watu wazuri katika kanisa la Kipresbiteri. Na mahali pote pale, ni wanaume na wanawake wanaongojea kuona hiyo Nuru ikimemetesha njiani mwao. Wewe endelea kumemetesha Nuru, katika unyenyekevu, uzuri. Hebu sisi sote tukue karibu zaidi na Mungu, kwa kujinyenyekeza. Mnaona?

⁴⁰ Msisahau, Maskani haya yatapoteza nguvu zake. Kumbukeni ya kwamba hili ndilo lengo ambalo shetani ameelekeza kila bunduki iliyo katika jehanum. Atamfanya mtu fulani afanye jambo ambalo ni kinyume na yale yule mwingine anawazia. Yeye anafanya jambo hilo. Yeye amelikazania. Hiyo ndiyo kazi yake, kama anaweza kumfanya mtu fulani kusema jambo fulani, mtu fulani kumsengenya mwingine, kusema, “Vema, hebu sikiza, unajua alilofanya *fulani*?” Usisikize hayo. Usisikize hayo, kamwe. Huyu ni ibilisi. Mnaona, ni Shetani. Usiamini jambo hilo.

41 Kama kuna jambo lo lote ambalo mtu ye yote amekosea, waombeeni. Na usiombe kichoyo, useme, “Najua ni wajibu wangu, yanipasa kumwomba ndugu huyo.” Litie ndani ya moyo wako, ndani kabisa, kwa ajili ya huyo dada. Na uzungumze tu na uwe mwema kabisa, na muda si muda, utawaona wakirudi ibadani tena. Mnaona? Maana, hata hivyo, tunaelekea kwenye machweo ya jua.

42 Bwana Yesu yuaja mojawapo ya siku hizi. Na, mwajua, nafikiri itatukia kwa ghafla sana ra—raha sana, hata kutakuweko na asilimia mia...moja kwa mia ya asilimia mia moja ya ulimwengu mzima hawatajua wakati huko Kunyakuliwa kutukiapo. Kutatukia kimya sana hata hakuna atakayejua neno juu yake. Mnaona?

43 Na kutakuweko, bila shaka, yale makundi madogo yatasema, “Vema, sasa, *Fulani?*”

44 “Loo, wao wanasema kuna kundi la washupavu wa dini kule, walisema kundi moja liliondoka likienda kutoka kule, nao... Hiyo si kweli. Wao wameondoka tu wakaenda mahali fulani. Tumekuwa na huo ushupavu wa dini, mnaona.”

45 “Vema, wanasema Maskani hayo madogo, katika mahali pamoja panapoitwa Jeffersonville, kulikuwa na washiriki wengi ambao hawapo tena.”

46 Mnaona, wanalipuuza tu jambo hilo. Watasema, “Loo, hakuna lo lote, mnaona,” namna hiyo, nako kutakuwa kumepita na hawatajua.

47 Kila mahali nchini, watakuja, waliokufa katika Kristo watafufuka kwanza. Kunyakuliwa kutatukia, Kanisa litatwaliwa Nyumbani. Nayo ile dhiki itaanza, na, loo, jamani, hatutaki kuwepo hapa wakati huo. Sitaki kuwa hapa katika ile Dhiki. La. Mungu azuie kwamba hata mmoja wetu asiwepo hapa wakati huo. Kwa sababu, “mwenye uchafu anazidi kuwa mchafu; na mtakatifu anazidi kutakaswa; mwenye haki anazidi kufanya haki.” Hakuna...Mwana-Kondoo alikuwa amekuja na Kitabu Chake cha Ukombozi, na Bibi-Arusi ameondolewa; wale waliopuuza hawana budi kupitia katika wakati wa ile Dhiki, Mataifa na Wayahudi pia. Ni wakati wa Dhiki jinsi gani! Siutaki huo.

48 “Bwana, nitakase sasa.” Hilo ni fundisho zuri la Kinazarayo, sivyo? [Ndugu Neville anasema, “Amina.”—Mh.] Na ni la kweli, pia. Ni la kweli. Hiyo ni kweli. “Nijaze sasa kwa Roho Wako Mtakatifu, Bwana. Utoe ulimwengu wote ndani yangu sasa, Bwana. Sitaki wo wote...”

49 Kama—kama alivyosema yule ndugu mweusi, “Bwana, nina tikiti yangu mkononi mwangu. Tayari imekwisha kutobolewa. Nitakapofikia kule chini mtoni, asubuhi ile, sitaki shida yo yote.”

50 Kwa hiyo, hiyo ni kweli kwa namna fulani, si—sitaki shida. Shika tikiti yako mkononi mwako, kwa maana tunavuka. Wazia tu jambo hilo, ule wakati mkuu wa ukombozi umekaribia.

51 Na sasa jambo lingine. Ndugu, anaitwaje, huku Utica? Nafikiri Ndugu Graham, na ndugu mwingine pale ambaye ni mchungaji pale. Kitu kama Ndugu Shanks ama kitu kama hicho, ama Sink? [Ndugu Neville anasema, “Ndugu Snelling.”—Mh.] Ndugu Snelling ndiye mchungaji, kwa jumla. Ndugu Snelling ndiye mchungaji huko Utica sasa. Nafikiri ibada yao ya maombi huwa mnamo . . . [“Alhamisi usiku.”] Alhamisi usiku. Sasa, mnajua, ni vema sana kama tungetelemka twende kule Alhamisi usiku na kuwaonyesha jamaa hao ushirika kidogo. Mnaona? Ndipo basi wakati Ndugu Jackson, wakati anapokuwa na wa kwake, kama tungekusanyika pamoja kikundi chetu kidogo kisha twende.

52 Endeleeni tu kuomba, endeleeni kuchimba! Naam, msikome. Ni kama tu wakati Eliya alipowaambia, kasema, “Chimbeni mahandaki pale!” Unaposhuka unaenda kule na kusikia mkebe wa kale ukisema, “Nimechoka sana,” utupilie mbali na uendelea kuchimba. Unaona? Endelea tu kuchimba, maana hatuna budi kuchimba. Hatuna budi kuchimba tu, ni hivyo tu. Maana, kama u—kama unatarajia kuepuka ile Dhiki, afadhali uanze kuchimba.

53 Sasa, kwangu mimi, ninajihubiria mwenyewe hapo. Nitaanza kuchimba ndani zaidi kuliko nilivyowahi kuchimba. Kwa maana, ninajisikia jinsi hiyo, nchini na duniani kote, kwamba huduma hii itafanya hivyo tena, kwa kuwa imejulikana sasa karibu kila mahali ulimwenguni. Si—sina budi kwenda tena.

54 Mke wangu aliniambia . . . juzijuzi asubuhi, nikasema, “Nataka uambatane nami nitakapoondoka. Nitaondoka mnamo Januari, Bwana akipenda. Nataka kufanya ziara ya ulimwengu mzima, kuuzunguka wote; nirudi na labda nifanye ibada Marekani, kwenye kama msimu ujao wa kiangazi.”

Ndipo akasema, “Mimi ni mzee sana kwenda.”

55 “Vema,” nikasema, “nimeenda nilipokuwa . . . juu ya safari yangu ya mwisho ya ng’ambo, yapata miaka minane iliyopita, nami najisikia kana kwamba niko katika hali bora zaidi ya niliyokuwa nayo miaka minane iliyopita unajua, unaona. Najua mengi zaidi kuhusu hilo sasa.”

56 Ndipo tukaanza kuzungumzia jambo hili, “Kama Bwana alisema, ‘Nitakupa miaka ishirini na mitano. Hutazeeka. Utaweza kwenda, nami nitakupa miaka ishirini na mitano duniani,’ ungechukua kutoka—kutoka kuzaliwa hadi ishirini na mitano, ama kutoka ishirini na mitano hadi hamsini, hamsini hadi sabini na mitano, ama sabini na mitano hadi mia?”

57 Sasa, mtu ye yote ambaye amepangiwa muda wo wote duniani, angefanya jambo la kijinga sana kama hatautumia wakati huo katika kazi ya Mungu. Sijali anafanya nini.

58 Naam, iwapo utakuwa wa kuwavunja moyo wanawake, na kadhalika, afadhali uchukue huo umri wa ujana mdogo, huo wa miaka ishirini na mitano ya kwanza. Unaona?

59 Iwapo utakuwa seremala, fundi wa mashine, ama cho chote kile, afadhali uchukue hiyo ishirini na mitano ya pili. Unaona?

60 Halafu nilikuwa ninawazia kuhusu, “Na mimi je, nitachukua wapi?” Ningechukua sabini na mitano hadi mia. Ninge kuwa mwerevu zaidi, mwenye hekima zaidi. Ninge kuwa nimetulia zaidi. Ninge kuwa na ujuzi zaidi wa yale ninayofanya. Niko na umri wa zaidi ya miaka kumi, minane ama kumi, kuliko wakati wa mwisho nilipokuwa katika nchi za ng’ambo. Siruki kama kwamba ninawaua nyoka. Nitajua mengi zaidi juu yake, mnaona. Ninajua jinsi ninavyo- . . .

61 Ni kama tu mbwa wa kuwinda wanyama wadogo akimshambulia mnyama huyo, mnaona, unajua jinsi ya kumshika. Usiruke mle ndani; atakukwaruza. Unaona, jifunze ujue mbinu zake na uangalie analofanya. Nasi tunajifunza mengi juu ya adui. Kwa hiyo hatuna budi kutafuta kujua mbinu zake zote, na jinsi anavyosogea, na yale afanyayo, na kujifunza makonde yake, ndipo basi umefunzwa kumkabili, unaona.

62 “Kwa hiyo naamini sasa,” nilimwambia mke wangu, “naamini niko katika hali bora zaidi sasa kuliko nilivyokuwa nilipokuwa na umri wa miaka arobaini, . . . ? . . .” Mnaona, nami nina umri wa miaka hamsini na minne. Nami naamini, kama nikiishi na ningali naweza kujimudu kama nifanyavyo sasa, nikiwa na umri wa miaka mia moja, kama niki- . . . kama Yesu atakawia muda huo, ninge kuwa na hali nzuri zaidi wakati huo kuliko niliyo nayo sasa, kwenda. Mnaona? Kwa maana, ungekuwa umejua mengi zaidi, ungejua ya kufanya vizuri zaidi, na jinsi ya kuliendea, jinsi ya kufanikiwa.

63 Chukua watu wengi sana sasa, kama watafanyiwa upasuaji. “Wanasema daktari mpya ambaye ndiyo kwanza ahitimu juzijuzi, ndiyo kwanza atoke katika chuo cha madawa. Hajafanya upasuaji bado. Hebu akufanyie.”

64 “Loo, la,” ungesema, “hakuna cha hiyo. Si jamaa huyo. La, bwana. Hata hivyo, la, hashu. Sitaki aniguse kwa kisu. Vema, afadhali nishuke niende huku nimpate *Fulani*. Nasikia amefanya upasuaji mwingi. Anajua jinsi ya kuufanya.” Naam basi, mnaona. Wazo ndilo hilo.

65 Unawazia haya, bali vipi kuhusu nafsi ile? Nataka mtu anayejua walipo, na anayejua barabara; mtu ambaye ameipitia. Ndiyo, bila shaka.

⁶⁶ Bwana awabariki. Sawa, Ndugu Neville, njoo hapa sasa. Na Mungu akubariki Ndugu Neville. Msisahau sasa, Jumapili ijayo.

⁶⁷ [Ndugu Neville anazungumzia juu ya Ndugu Branham na Ndugu Vayle kwa dakika moja, kisha anasema, “Nami nafurahia kuwakaribisha wahudumu wa Mungu, hasa sana hao wanaoshirikiana na Hili, na katika Hili pamoja nasi. Nafurahia sana kusikia kutoka kwao.”—Mh.] Amina. [“Kwa hiyo nilimwomba Daktari Lee Vayle, nilisema, ‘Je, ungeweza kuhudumu kama Ndugu Branham hatahudumu?’ Naye Ndugu Branham hakuhudumu. Huenda alijua jambo hili.”]

La, hakujua, ama kweli hata nisingalinena kwa muda huo wote.

⁶⁸ [Ndugu Neville anasema, “Kwa hiyo nilimwomba Ndugu Vayle, usiku wa leo, iwapo atatuhudumia, pindi Ndugu Branham hatafanya hivyo. Kwa kuwa alishirikiana naye mikutanoni, naye anaijua ile Njia, Njia hii. Nasi tunafurahia kuwa na Ndugu Vayle. Ninamthamini na kumheshimu jinsi ninavyofanya kwa ye yote wa hao wahudumu wengine, na kama ninavyowaheshimu wengine wote. Na kwa hiyo iwapo atakuja usiku wa leo na kutuzungumzia, ningefurahiwa akifanya hivyo.”—Mh.] Amina. [“Mungu akubariki, na hebu tumwombee Ndugu Vayle. Wengine wenu hawajamsikia, nami natumaini mtamwombea.”] Ndiyo.

⁶⁹ Nisingechukua wakati wake wote. Nawaomba makutano msamaha. Sikujua, nikiketi pale, kwamba yeye... hii ilikuwa imepangwa. Mungu akubariki, Ndugu Vayle.

⁷⁰ [Ndugu Lee Vayle anasema, “Haikuwa imepangwa. Yeye alisema, kama wewe ‘hukunena.’ Nawe ukaja.” Ndugu Branham na kusanyiko wanacheka—Mh.] Sawa. Hilo ni sawa.

⁷¹ Mimi humsikia, mimi mwenyewe. Ndugu Vayle amezungumza mara nyingi mbele yangu, mikutanoni, na—na kadhalika. Yeye aliiongoza mikutano kwa muda mrefu, na ni ndugu mzuri, amefanya kazi ya kufana sana. Nami nina hakika kusanyiko hili daima linafurahia kumsikia Ndugu Vayle anapozungumza. Bwana akubariki Ndugu Vayle.

⁷² [Ndugu Vayle anazungumza kwa dakika sabini juu ya Marko 16:15-20 na Maandiko mengine, kichwa chake: *Kwa Nini Marko 16 Haijatenda Kazi? Na Jinsi, Kulingana Na Maandiko, Ya Kuifanya Itende Kazi*—Mh.]

⁷³ Mengi sana yalisemwa hata ni—ni—nisingesema lo lote kuyafanya bora zaidi. Nami naamini kweli ilikuwa ni Bwana aliyemwezesha Ndugu Vayle kuuleta ujumbe huu, baada ya asubuhi ya leo. Maana, unaona, haina budi kutenda kazi namna hiyo. Tu—tunakubali hilo kutoka kwa Mungu. Yale, kuna mambo mengi sana aliyokuwa anasema; ni—ni—nilikuwa na masomo ishirini yaliyoandikwa hapa sasa hivi, yale aliyosema.

⁷⁴ Nilikuwa nikifikiria hapa juu ya mfano mmoja mdogo, kuunga mkono aliyosema. Sasa, tunaangalia saa hii, tujue ni saa ngapi. Isipokuwa kila kidude katika saa hiyo kiwe kinashirikiana, kimoja kwa kingine, hatutajua kamwe ni saa ngapi. Sivyo? [Kusanyiko, "Amina."—Mh.] Na hiyo inahitaji sisi sote, wote pamoja, iwapo kweli tunataka kuona ule Mvuto wa Tatu ukitenda jambo fulani kwa ajili ya Mungu, tushirikiane na kila mmoja wetu, tujinyenyekeze mbele za Mungu na kutubu makosa yetu, na kumwomba na kumwamini Mungu kwa ajili ya mambo haya.

⁷⁵ Kweli naamini yale aliyosema Ndugu Vayle ni Kweli, ya kwamba Mungu hataweka kamwe Roho Wake katika hekalu lisilo takatifu, lisilo safi, lisilotii. La. Haina budi kuja kwa—kwa njia ya kuisafisha mioyo yetu na hila zote na uovu, kusudi tuwe wasafi mbele za Mungu, kusudi apate kumwingiza Roho Wake Mtakatifu na msafi ndani yetu, kuyatimiliza mambo haya. Na—nafikiri ya kwamba, mtakapoenda nyumbani usiku wa leo, kama mtakisoma hicho Kitabu kidogo cha Yuda, mtajifunza mengi sasa ya yale Ndugu Vayle amesema. Naye alisema, "Naishindania imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu." Wao waliiacha. Jinsi watu walioharibika akili zao, na kadhalika, walikuwa wamekuja wakawadanganya wakawaondoa kutoka kwa—kwa mambo yote halisi ya Mungu.

⁷⁶ Na Mungu anaweza tu kutenda kazi tunavyomruhusu atende. Na kuna mambo mengi ya ajabu, ninayosema . . .

⁷⁷ Mnajua, watu wanataka nguvu, na kwa kweli hawajui nguvu ni kitu gani. Mnaona, kweli ha—hawajui ki—ki—kinachoambatana nazo. Nji—njia ya kupanda juu ni kushuka chini, daima. Kama unataka nguvu, angalia unavyoweza kuwa mnyenyekevu. Ondoka tu kwenye mawazo yako yote ya kilimwengu, na ujinyenyekeze mbele za Mungu, ndipo una nguvu kuliko mtu anayekimbia huku na huko jengoni na kufanya kelele nyingi; unaona, kwa maana umeweza kujishinda mwenyewe, na kujikabidhi kwa Kristo, unaona, kujinyenyekeza mbele Zake. Hiyo ni nguvu kweli.

⁷⁸ Hebu nionyeshe kanisa ambalo ni nyenyekevu, nyenyekevu kabisa, halina ma—majivuno; kanisa, kanisa zuri na nyenyekevu, nitakuonyesha kanisa ambalo lina kibali na nguvu za Mungu ndani yake. Hiyo ni kweli. Hilo ndilo linalohitajika, unye- . . . unyenyekevu, kujinyenyekeza mbele za Mungu, kumruhusu Mungu afanye kazi kupitia kwetu sisi. Si lazima ufanye kelele nyingi.

⁷⁹ Wakati mwingine, kama alivyosema yule mkulima, alienda shambani na gari lake la kukokota, na, kila alipokanyaga shimo, lilitatarika na kuendelea. Bali aliporudi, alipitia kwenye shimo lile lile na halikufanya kelele yo yote, kwa maana lilikuwa limepakwiwa vitu vizuri.

⁸⁰ Kwa hiyo nafikiri hilo ni kama sawa tu, mnaona, kwamba tunajazwa na mambo mazuri ya Mungu, ili kwamba tunda la Roho lipate kujulikana kupitia kwetu. Kama alivyorejea mara nyingi kwenye Wakorintho wa Kwanza 13 pale, na jinsi, kwamba, “Nikijitoa mwili wangu niungue moto, na nina mambo haya yote, na sina upendo; ni bure, hainifaidii kitu.” Mnaona, tunataka kufanya jambo hilo.

⁸¹ Juu ya mambo yote, wajibu wetu mbele za Mungu ni nafsi zetu sisi wenyewe. Mnaona, ni—ni *wewe* unayekwenda Mbinguni. Si kama *mimi* nitaenda, ama *yeye* ataenda. Ni *wewe* unayekwenda, unaona, nawe kwanza. Na huna budi kuchunguza jambo hili kwanza kisha uje ukiwa mwema mbele za Bwana.

⁸² Na daima nimeona kwamba mtu ajidhiliye ndiye mtu ambaye Mungu atamkweza. Ukimchukua mtu mwenye kifua mbele na mjuvi, na huwezi kumwambia kitu, ni mwenye kiburi, na—na, vema, huyo—huyo ndiye mtu ambaye hafikii po pote. Bali hebu umchukue mtu ajidhiliye na ana mwenendo mzuri.

⁸³ Nilikuwa nikizungumza na mtu fulani hivi majuzi, ambaye anaendeleza kanisa kule kwenye . . . alitoka kwenye madhehebu yaliyokuwepo. Na, vema, ni Ndugu Boze, na hayo makanisa ambamo walikuwa, walikuwa na kanisa hilo kubwa pale kwa muda mrefu sana, naye Bwana alikuwa anawabariki. Ndipo watu wakafikia mahali ambapo walitaka kujiadibisha kama hao wengine, nao walitaka kulitupilia kwenye madhehebu. Nao walipofanya jambo hilo, ilininino tu . . . hao Wakristo wanyenyekevu mle ndani hawakutaka jambo hilo. Maishani mwao mwote, walifundishwa dhidi yake, kwa hiyo wakaliacha tu. Sasa wana kundi, na Bwana amewabariki sana hata wanaingia, sasa wanafikia mahali pa kuwa wakubwa tena, kwa kanisa ambalo linachukua watu elfu nne ama elfu tano, nao wanaanza tena.

⁸⁴ Nao wakanijia, wakasema, “Ndugu Branham,” wameketi pale pale afisini, afisi ya kanisa, juzijuzi. Kisha akasema, mmoja wa hao viongozi, Ndugu Carlson na hao wengine, kasema, “Tufanye nini?”

⁸⁵ Nikasema, “Mtafuteni mtu awe mchungaji ambaye hana sifa katika madhehebu yote, ambaye kweli ni ndugu mzuri, wa kweli, mwema na mnyenyekevu ambaye anaishi maisha mazuri. Mungu atashughulikia mengine yote, mnaona.” Nikasema, “Mchungaji mzuri ambaye atawalisha kondoo na kuwa mnyofu na kadhalika, Mungu atashughulikia yale mengine yote. Kama uta . . . Si mjuvi fulani mkubwa aje, ati anataka kutengeneza *hili*, na eti hili linapaswa kuwa namna *hii*, na kukatakata mambo kila mahali.” Nikasema, “Haitafulu. Ndiyo kwanza mpitie hayo.”

⁸⁶ Naam, kila kipande kanisani hakina budi kufanya kazi pamoja, nawe huna budi kudumisha sehemu yako. Kwa

hiyo tunaona wakati tunaoishi. Huenda tumekaribia kuliko tunavyodhania tumekaribia.

⁸⁷ Sasa, tunamthamini Ndugu Vayle. Sivyo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Bwana akubariki, Ndugu Vayle. Asante. Nasi tunamshukuru Mungu kwa kutuletea ujumbe huu mkuu usiku wa leo.

⁸⁸ Nami nilipata kijikaratasi chenye maandishi, dakika chache zilizopita. Mmoja wa akina dada amekuwa na jambo fulani alilokuwa anataka kusema, katika ndoto. Kama tu utaniandikia, dada, mi—mimi. . . Yeye amempa ndoto ambazo zimekuwa za kweli kabisa. Hatukubaliani na ndoto zote. La, la. Bali zinapokuwa za Mungu, tunataka kujua ya kwamba ni Mungu anayezungumza nasi.

⁸⁹ Kama vile kila kitu kinachozungumza kwa lugha, hatukiamini; bali wakati fasiri inapotokea inayotwambia jambo litakalotukia, tunalionga likitukia, ndipo tunamshukuru Mungu kwa sababu ya hilo. Mnaona?

⁹⁰ Tunataka kuliacha likiendelea vyema, vizuri, na katika utaratibu wa Mungu. Kwa hiyo kumbuka tu, ya kwamba sehemu yako huenda ikawa ni kamani kuu, ama yaweza iwe ule mdogo, mkono fulani mdogo, ama sehemu ndogo, ama kile kidude cha kutia majira, hata iwe nini, ama labda ile mikono kwenye uso wa saa, ambayo huonyesha saa. Lakini hata iwe nini, tunahitajiwa kwamba sote tufanye kazi katika moyo mmoja na Injili ya Yesu Kristo, kulifanya hili litimie.

⁹¹ Hebu wazia! Kama vipawa ni vikubwa namna hiyo, tunayoita nguvu; naye Paulo alisema, “Nijapokuwa na imani hata ningehamisha milima, na sina upendo, si kitu mimi.” Wazia jambo hilo.

⁹² Na hata ingawa sisi husema, “Vema, ingawa na—nafahamu. . . Laiti ningaliijua Biblia.”

⁹³ “Nijapofahamu siri zote za Mungu, mnaona, na hata hivyo nijapozifahamu na niwe sina upendo, si kitu mimi. Unaona, sijafikia po pote bado.” Mnaona, jambo muhimu ni kwamba, mpende Mungu, na ujinyenyekeze kwa jambo hilo.

⁹⁴ Sasa, hakika, baada ya miaka hii yote uwanjani na kuuzunguka ulimwengu, na kuwaona watu mbalimbali, napaswa kujua kidogo juu ya lango la kuingilia. Na iwapo unataka kufikia po pote na Mungu, usiruhusu kamwe roho wa kiburi akukaribie. Usiruhusu uovu wo wote ukuingie. Haidhuru mtu mwingine ye yote anafanyaje, kama wamekosea, usijifanyie kinyongo dhidi ya mtu huyo. Unaona? Wewe uwe mtu mzuri na mwenye fadhili. Kumbuka, Mungu alikupenda ulipokuwa dhambini. Na iwapo Roho wa Mungu yuko ndani yako, unampenda mtu huyo mwingine wakati amekosea. Unaona, waombee tu, na mpendane nyinyi kwa ninyi.

⁹⁵ Juu ya yote, mpende Mungu na mpendane ninyi kwa ninyi. Na mwe wanyenyekevu kwa Mungu na mmoja kwa mwingine, na Mungu atalibariki jambo hilo, na ni vigumu kusema atakalofanya. Kwa kawaida kanisa linapoanza kuongezeka na kuanza kuwa kubwa zaidi, ama kitu kama hicho, ndipo wanakiacha kitu kilicho halisi, kitu halisi.

⁹⁶ Mnajua kilichosababisha mambo haya, wakati nilipoanza kwanza na Bwana akanitokea kule chini mtoni na kuniambia jambo hilo? Na Ndugu Vayle aliona jambo hilo, naamini, katika gazeti moja kule Canada, miaka mingi iliyopita, ambapo Malaika wa Bwana alitokea chini kule mtoni, na ilikuwa kwenye Associated Press, “Nuru isiyoeleweka juu ya mhudumu wa huo mtaa, huku anabatiza.” Na—na mnajua kilichosababisha jambo hilo? Tulipokuwa na mkutano wa hema upande wa pili wa barabara ya mji, hema ambayo iliwachukua yapata, loo, watu elfu mbili mia tano, wahudumu walitoka kila mahali, wakasema, “Ndugu, njoo hapa kidogo.” Nilikuwa tu kijana, kama, loo, mtoto tu. Nao wakasema, “Unawadumishaje hao watu kwa moyo mmoja? Wanapendana wao kwa wao hata . . . Sijaona watu wanaopendana.”

⁹⁷ Huyu ni Bwana. Hili kanisa lilianzishwa juu ya jambo hilo, huo upendano wa kiungu na wa kindugu mmoja kwa mwingine. Niliwaona hata wakisalimiana wao kwa wao, wakiondoka mahali hapo, na kulia kama watoto wachanga, kwa kuachana. Wanapendana vizuri namna hiyo. Nami ningeenda manyumbani mwao kuwatembelea, na wakati mwingine Biblia ilikuwa imefunguliwa huku imejaa alama za majonzi. Nikaingia, wakati wa usiku, ambapo mama na baba walikuwa wamekusanyika pamoja, na watoto wao wadogo hapo sakafuni, wamepiga magoti; na baba na mama wanapiga magoti, wanalia na kuomba. Ningesimama mlangoni nikangoja na kungoja na kungoja. Nao hawakuacha kuomba, nitakaa chini kwenye vipandio na kuanza kuomba, mimi mwenyewe, huku ninawangojea, mnaona. Na hivyo—ndivyo ilivyokuwa. Nao walipendana. Walipendana. Tulikuwa tunasimama na kuimba ule wimbo wa kale:

Kibarikiwe kifungo kiifungacho
Mioyo yetu katika upendo wa Kikristo;
Ushirika wa nia moja
Ni kama wa kule Juu.

Tunapoachana,
Hutuhuzunisha kindani;
Bali bado tutakuwa tumeunganishwa miyoni,
Na kutumaini kukutana tena.

⁹⁸ Nasema jambo hili nikiwa na furaha kuu moyoni mwangu, kwa Kristo; wengi wao wamelala huku katika makaburi haya yaliyoandikwa usiku wa leo, wakiungojea ule ufufuo mkuu ambapo tutakutana tena.

⁹⁹ Hebu Roho huyo asiondoke mahali hapa! Kama akiondoka kamwe, basi sijali jinsi mchungaji wenu alivyo na ufasaha wa lugha, jinsi anavyoweza kulileta Neno la Mungu vizuri, Roho wa Mungu amehuzunishwa akaondoka. Mnaona? Wakati tunapoweza kuwa na mambo yote katika ushirika, pamoja, na kupendana sisi kwa sisi, ndipo Mungu atatenda kazi pamoja nasi.

¹⁰⁰ Nasi tunatunza wakati, ili kwamba watu watakuja huku na kusema, “Kama ukitaka kuona kanisa ambalo kweli ni nyenyekevu, kanisa ambalo kweli linampenda Mungu, nenda kule kwenye yale Maskani wakati mmoja na kulitazama. Tazama wanavyopendana, ile heshima; wakati Injili inahubiriwa, jinsi walivyo na uchaji, jinsi kila kitu kiko katika utaratibu.” Naam, ndipo wanaweza kuangalia na kuona ni wakati gani tunaishi. Mtaona Roho wa Bwana akitenda kazi kati yenu, ishara kubwa na maajabu yatakuwa yakitendeka. Kama hicho kitu kinafanya kazi pamoja, kinaonyesha saa. Bali kama hakitendi kazi, basi saa imesimama, hakitaonyesha saa tena. Kwa hiyo tukitaka kujua ni wakati gani tunaishi, hebu kila mtu na aanze kufanya kazi pamoja katika Injili, wakipendana, wakimpenda Mungu, ndipo mikono yenyewe itaonyesha saa tunayoishi. Mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Bila shaka. Amina. Bwana awabariki, kwa wingi.

¹⁰¹ Msisahau sasa, tembeeni kila mahali juma hili. Na kama mnawajua watu wote wazuri walio wagonjwa na wanakuja humu, waambieni, watakapokuja, useme, “Mpendwa, nataka kukuuliza. Tunawaombea wagonjwa, Jumapili asubuhi, huko kwenye Maskani. Nawe umekuwa mgonjwa kitambo, sasa nataka . . .

“Vema, nataka kwenda. Daima nimetaka kwenda.”

¹⁰² “Sasa, ndiyo kwanza nisikie ujumbe Jumapili iliyopita usiku, kutoka kwa ndugu fulani pale, jinsi itupasavyo kuungama makosa yetu sisi kwa sisi, na kuombeana, kusudi tupate kuponywa. Yakobo 5:14, 13, 14, 15, mnaona, ya kwamba hatuna budi kuungama makosa yetu sisi kwa sisi kabla hata hatujaja tupate kuombewa. Naam. Kuungama makosa yetu sisi kwa sisi, na kuombeana.” Mnaona? Mnaona, hilo ndilo alilokuwa akizungumzia hasa usiku wa leo, akizichanganya zile heri na Marko 16. Zichanganyeni hizo pamoja, mmezipata, basi kuponya kunatukia.

¹⁰³ Mwangelie Yesu, hakuna kitu ila bunda moja la upendo. Mnaona? Alikuwa Mungu aliyedhirishwa. Yeye, Mungu, alijionyesha kupitia Kwake, si ajabu miujiza na kadhalika ilitendeka. Maisha Yake manyenyekevu, na maisha yaliyowekwa wakfu; alipojishusha kutoka kuwa Mungu, awe mwanadamu hapa duniani, kumwonyesha Mungu kupitia kwa Nafsi Yake. Hicho ndicho kilichomfanya alichokuwa. Daima

nimesema, “Kilichomfanya Yesu Mungu, kwangu mimi, ni jinsi alivyojinyenyekeza. Yeye alikuwa mkuu sana, na hata hivyo aliweza kuwa mdogo sana.” Mnaona? Hiyo ni kweli.

¹⁰⁴ Bwana awabariki sana. Sasa na tusimame, kwa ajili ya kuwaacha mfumukane. Basi na tujaribu huo, (huenda ikawa huujuu, dada), huo, *Kibarikiwe Kifungo Kitufungiacho*. Hebu na tuuimbe huo mara moja, sivyo? Hebu tupe sauti.

Kibarikiwe kifungo kitufungiacho
Mioyo yetu katika upendo wa Kikristo;
Ushirika wa nia moja
Ni kama wa kule Juu.

¹⁰⁵ Sasa huku tunapoimba kifungo hiki cha mwisho, na tushikane mikono sisi kwa sisi, “*tunapoachana*,” na kusema tu, “Mungu akubariki, ndugu, dada. Ninafurahia sana kuwa hapa pamoja nawe usiku wa leo.” Mnaona, kitu kama hicho, kisha mgeuke tena. Sasa hebu na tuuimbe.

Tunapoacha... (Mungu akubariki, Ndugu Neville)
Hutuhuzunisha kindani;
Bali bado tutakuwa tumeunganishwa mioyoni,
Na kutumaini kukutana tena.

¹⁰⁶ Jinsi tunavyompenda Bwana Yesu! Sivyo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Jinsi...

Hata twonane huko juu!
Hatatwonane Kwake kwema; (Kwake kwema!)
Hata twonane huko juu!
Mungu awe nanyi daima!

Hebu na tuyafunge macho yetu, na tuimbe tu huo kwa Roho sasa.

Hata twonane huko juu!
Hata twonane Kwake kwema;
Hata twonane huko juu!
Mungu awe nanyi daima!

¹⁰⁷ Sasa huku vichwa vyetu vimeinamishwa. Sisi ni watoto tu, watoto wa Mungu. Hebu na tuuvumishe. [Ndugu Branham na kusanyiko wanaanza kuuvumisha, *Mungu Awe Nanyi*—Mh.] Loo, jinsi huo unavyomleta Roho wa Mungu kwetu! Ungewazia siku za mwanzoni walipoketi juu ya bamba za miamba?

Mungu awe nanyi daima!

¹⁰⁸ Huku vichwa vyetu vimeinamishwa, nitamwomba Ndugu Allen nyuma huko, ndugu aliye mgeni miongoni mwetu, kama ataturuhusu tufumukane kwa maombi. Ndugu Allen.



JINYENYEKEZE SWA63-0714E
(Humble Thyself)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili jioni, tarehe 14 Julai, 1963 katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1992 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org